

## 13- Miyqaat

Miyqaat ni mipaka iliyoko sehemu nne inayozunguka Makkah. Yeyote atakayeivuka bila ya kuingia katika Ihraam atakuwa hakutimiza moja wa nguzo za ‘Umrah na Hajj, itabidi arudi kwenye Miyqaat ili ahirimie huko. Akishindwa hivyo basi Wanachuoni wengi wameona kwamba itabidi aliye kaffaarah ya kuchinja na kugawa nyama yake kwa masikini wa Makkah kwa sababu ameacha kutekeleza kitendo cha waajib.

Rasuli (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) alidhihirisha mipaka hiyo kama ifuatavyo:

عَنْ إِبْرَاهِيمَ (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا): أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَقَتَ لِأَهْلِ الْمَدِينَةِ: ذَٰلِكُ الْحُلَيْفَةُ.  
وَلِأَهْلِ الشَّامِ: الْجُحْفَةُ. وَلِأَهْلِ تَجْدِيدِ قَرْنَةِ الْمَنَازِلِ. وَلِأَهْلِ الْيَمَنِ: يَلْمَلَمُ هُنَّ هُنَّ وَلِمَنْ أَتَى عَلَيْهِنَّ مِنْ  
غَيْرِهِنَّ، مِنْ أَرَادَ الْحَجَّ أَوْ الْعُمْرَةَ. وَمَنْ كَانَ دُونَ ذَلِكَ: فَمِنْ حَيْثُ أَنْشَأَ، حَتَّىٰ أَهْلُ مَكَّةَ مِنْ مَكَّةَ.

Imepokelewa toka kwa Ibn ‘Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba: “Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ameweka Miyqaat kwa ajili ya watu wa Madiynah kuwa ni Dhal-Hulayfah. Watu wa Shaam ni Al-Juhfah. Watu wa Najd ni Qarnal-Manaazil na watu wa Yemen ni Yalmama. Miyqaat hizo ni kwa ajili ya wenyehi wa huko na wengineo wenyehi kuzipita kwa anayetaka kufanya Hajj au ‘Umrah. Na anayeishi katika maeneo hayo anaweza kuingia Ihraam katika sehemu anayoanzia hata watu wa Makkah waanze Ihraam zao kuanzia Makkah.”<sup>1</sup>

Kwa maana kuwa, ukiwa unatoka Afrika Mashariki sehemu yako ya kuhirimia ni Yalamlam kama unaelekea Makkah moja kwa moja. Lakini ikiwa mathalani Mahujaji watakwendwa Madiynah kwanza kwa ajili ya kuzuru Msikiti wa Rasuli (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) kisha ndiyo baadaye waende Makkah kwa ajili ya Hajj, hapo sehemu ya kuhirimia itakuwa ni ile ya watu wa Madiynah yaani Dhul-Hulayfah na si ile ya kawaida waliopangiwa yaani Yalamlam.

---

<sup>1</sup> Al-Bukhaariy.

<b>Miyqaat</b>	<b>Eneo Na Umbali Wake (takriban)</b>	<b>Mahuaji Kutoka</b>
Dhul-Hulayfah	Kilo mita 450 Kaskazini ya Makkah (Kilomita 10 nje ya Madiynah)	Mahuaji wa kutoka Madiynah na Kaskazini.
Dhaat-'Irq	Kilo mita 94 Kaskazini-Mashariki ya Makkah	Mahuaji wa kutoka pande za Iraq.
Qarn Al-Manaazil	Kilomita 94 Mashariki ya Makkah.	Najd.
Yalamlam (As-Sadi'ah)	Kilomita 54 Kusini ya Makkah	Hii ni kwa ajili ya watu wanaotoka Yemen na pande za Kusini. (Afrika Kusini, Nigeria, Afrika Mashariki, Afrika ya Kati).
Al-Juhfah	Kilomita 197 Kaskazini Magharibi ya Makkah karibu na mji wa Rabiygh	Mahuaji kutoka Shaam (Syria, Jordan, Palestina, Egypt na pande hizo. Vilevile USA, Canada na UK).



### Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa

- Mahujaji wengine wanavuka *Miyqaat*, kituo kilichoteuliwa kwa ajili kuhirimia katika njia za msafara wao bila ya kuwa katika Ihraam hapo. Wanaendelea hadi wanafika Jeddah au sehemu nyingine katika mipaka ya vituo ambako huko ndio wanaingia katika Ihraam. Hivi ni kinyume na amri ya Rasuli wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) ambayo inaanrisha kuwa kila Haaj anapaswa ahirimie katika *Miyqaat* iliyoko katika njia ya msafara wake. Inapomtokea mtu hivyo, ni lazima arudi

katika *Miyqaat* yake, aingie katika Ihraam. Au itambidi afanye *kaffaarah* kwa kuchinja kondoo atakapokuwa Makkah na kuigawa nyama yote kuwalisha masikini. Hii inawahu su Mahujaji wote, wanaopita *Miyqaat* wakiwa wamesafiri kwa njia ya angani, bahrini au nchi kavu.

- Baadhi ya Mahujaji wanaosafiri kuingia Jeddah, wanaingia Ihraam Jeddah wakidhania kuwa ni *Miyqaat*. Haipasi kabisa kwani ni kuvunja kanuni ya Ihraam. Anayeingia katika Ihraam Jeddah, ni wakazi wake pekee wanaotakiwa kuingia Ihraam majumbani mwao. Mahujaji hutangaziwa wakiwa angani, dakika chache kabla ya kufikia mpaka wa *Miyqaat* ili watie niyyah zao za Ihraam.
- Kutoka nje ya *Miyqaat* kila siku kwa ajili ya kufanya ‘Umrah. Ingawa inaruhusiwa, ila inasababisha zahma kuzidi katika Masjidil-Haraam kwenye Twawaaf na As-Sa’-y.